Kundi cha Uzima: Mambo ya kutenda

Nao wataitwa mialoni madhubuti,
aliyopanda Mwenyezi-Mungu
kuonesha utukufu wake.
Watayajenga upya magofu ya zamani,
wataisimika miji iliyoharibiwa hapo kwanza.
Isaya 61:3-4

Kundi cha uzima kinawaunganisha watu toka misingi mbali mbali na eneo tofauti za kijiji. Kinafunza ukweli wa Yesu kwa kila mmoja na kutenda kwa pamoja kuboresha maisha kwa kila mtu. Kama mitende iliyoimarishwa kwa haki yake Mungu, wanakuwa wajenzi wa Jamii kwa upendo na ukweli katika kijiji chako.

Dunia inakabiliwa na dharura ya matibabu. Waweza hisi kwamba uko mbali na Miji mikubwa hivo haijalishi, lakini yajallisha maana wote twahitaji kuchukua taadhari. Kuenezwa kwa virusi/ugonjwa wa COVID-19 yamanisha kwamba tutaweza kuyafanya Makundi ya Uzima tofauti kwa mda. Kijikaratasi hiki kinakufahamisha jinsi ya kuongoza Kundi cha uzima wakati huu wa janga. Pia waweza angalia kijikaratasi kinachafunza 'COVID-19 Ni Nini' na kuelezea ugonjwa huu. Kijua ugonjwa huu itawasaidia watu kufahamu kwamba haijatokana na Mungu, na pia sio laana au uchawi.

Pamoja

Tujitahidi kushughulikiana kwa ajili ya kuongezeana bidii ya kupendana na kutenda mema. Tusiache ile desturi ya kukutana pamoja, kama vile wengine wanavyofanya.

Waebrania 10:24-25

Kirusi cha COVID-19 Kinaambukizwa mtu mmoja hadi mwingine wakiwa karibu. Twapaswa kuyaongoza makundi kwa njia isiyo atarisha watu kuambukizana virusi hivi. Tuna jukumu la

mmoja hadi mwingine na kijiji chetu. Twahitaji kumutegemea Yesu na tuzidi kupendana.

Ushauri wa huduma ya afya wapaswa kufuatwa wazi. Makundi huenda yakome kukutana. Iwapo hivo kiongozi aweze kutumia rununu (simu) barua fupi ama mtandao kuhakikisha kila mtu yuko sawa. Kumbuka mwaweza fanya kazi pamoja kwa uaminifu na kwa wema wa kila mmoja iwapo mwaweza kutana pamoja.

Iwapo Kundi cha Uzima chaweza kukutana, watu hawapaswi kuguzana kwa njia yeyote. Kusanyika inje ama kwenya Kanisa kubwa au darasa kubwa ambapo kila mtu atakaa peke yake kwa hatua tatu kubwa kutoka kwa mwingine.

Salamu za mkono au kukumbatiana inashurutishwa. Hapana kutumia chombo kimoja kati ya watu wawili au zaidi ya mtu mmoja.

Iwapo mtu ni mgonjwa, kohozi, homa ama hajihisi nafuu kwa namna yeyote, hapaswi kuudhuria kundi.

Omba

Salini daima, mkiomba msaada wa Mungu. Salini kila wakati kwa nguvu ya Roho. Kesheni bila kuchoka mkisali kwa ajili ya watu wote wa Mungu.

Waefeso 6:18

Ni muhimu sana kuweza kuombea kijiji chako na maeneo yako wakati huu. Muombee kila mmoja bila kujali tabaka, kabila au dini. Tunayo jukumu kumuombea kila mtu.

Mawazo

Kwenye Kijiiji chako, kunaweza kuwa na watu wagonjwa wa maradhi haya au kitu kingine. Unaweza watembelea mradi tu uweze kujitenga na marafiki zako na pia usiingie ndani ya nyumba wanayoishi. Waweza kuwaombea kwa sauti ukiwa nche bila kuwaguza. Haijalishi hali gani haupaswi kumuombea mtu na kumuekelea au

Dignity ni Shirika halali nambari 1122656. Dignity (Worldwide) ni kampuni ndogo na dhamana, imesajilliwa katika Uingereza na Wales nambari 6394480.
Dignity Zambia Ltd is a Public Benefit Company, registered in The Republic of Zambia No. 117117 | Biblia Habari Njema kwa Watu Wote (Yenye Vitabu vya Deuterokanoni): Tafsiri ya Ushirikiano wa Makanisa (BHN): Hakimiliki - 1995, 2001: kwa Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

kumuguza kwa mikono. Maanake kumuguza mtu ni mojawapo ya njia virusi hivi vinaambukiza.

Watu waweza ombeana kwa njia ya mitandao kwa barua fupi ama makundi ya mitandao. Mtu mmoja anaweza pitisha vipengele nya maombi kwa watu wengine nyumbani mwao ama wote waweza omba kwa wakati mmoja. Wakati wamaombi watu waweza asha taa kama ishara kuwa wanaombea kijiji.

Ukweli

Lakini mwenye kuuzingatia ukweli huja kwenye mwanga, ili matendo yake yaonekane yametendwa kwa kumtii Mungu.

Yohane 3:21

Kila mmoja anaeza endelea kujifunza kweli muhimu wa Yesu pamoja. Tunapenda watu na vijiji karibu nasi kujua ukweli na kujua Yesu. Wanaeza mtegemea haswa wakati huu, kupata amani na ukweli.

Mawazo

Watu wanaoandaa kundi waweza yapeleka mafunzo kwenye kijiji. Wanafaa kuzingatia kwamba hawaguzani na mtu. Popote palipo na nyumba kwa pamoja wanaeza funza kwa sauti na kujadiliana na watu. Hii isipowezekana, waandalizi waweza pia enda nyumba moja hadi nyine wakifunza. Hawapaswi kuingia ndani ya nyumba , kushiriki kinywaji ama kumugusa yeyote nyumbani.

Iwapo watu watokomeshwa kutembeleana, basi ujumbe fupi, kupiga simu au mtandao yaweza tumika katika hali hii. Yawezekana pia usiweze shiriki kila kitu, bali andiko tu tutoka kwa muongozo kisha uwaulize watu maoni yao. Muombe Mungu akuonueshe vipengele muhimu kila wiki.

MTANDAO

Kwa ujumbe zaidi jinsi ya kuhusika na Dinity, mafunzo, ushauri ingia kwa mtandao.

Upendo kwa wote

Wapenzi wangu, tupendane, maana upendo hutoka kwa Mungu. Kila mtu aliye na upendo ni mtoto wa Mungu, na anamjua Mungu.

1 Yohane 4:7

Kuapenda watu ni muhimu. Twaweza jiona kama masikini au hatuwezi kufaulu. Hii sio kweli. Tuna uwezo wa kumujali mtu. Ni vyema kuangalia mahitaji yetu lakini twapaswa kuangalia mahitaji ya wengine pia.
Tunaweza fanya hivi vipi wakati huu?

Mawazo

Wasaidie watu! Iwapo mzima na wa afya njema waeza enda sokoni ama dukani kumusadia mtu umri au mtu ambaye ni mgonjwa. Waweza acha chakula au maji kwa mlango wa mtu. Waweza saidia kwa mimea au shamba la mtu pasipo kutarajia kulipwa.

Iwapo watu wapaswa kukaa pekee yao kuna uwezekano wahisi upweke na ukiwa. Waweza wahimiza kwa ujumbe fupi ama kuwaongelesha nje ya nyumba zao. Shiriki kifungo kutoka kwenye bibilia, peana mda wako na jenga urafiki. Kumbuka kusisimama hatua tatu kutoka kwa mwenzako.

Wasaidie watu kufamu kwamba hawapaswi kufadhaika.
Kuna amani na faraja kwa Mungu. Maisha haya hayakomi iwapo tunamujua Yesu. Tunaweza wasaidia watu kujua uwkeli huu wenyewe.

Shiriki ufahamu ulionao kuhusi nini kinatendeka na magonjwa haya ya COVID-19. Hii itawasidia watu kuelewa bali sio kushutuliwa na ujumbe usio kamili.

KUMBUKA: KILA MARA FUATA USHAURI WA SERIKALI NA IDHARA YA AFYA

Pata ufikiaji kwa mtandao wa:
www.dignityonline.org.uk/publications

Mwongozo iliyoundwa kwa Metro Icon Studio 5 Iliyochapishwa na SyncFusion. Icon Kutumika Kwa idhini. Utukope twa Kulangilila twapangilwe naba Metro Icon Studio 5 abatulembele niba SyncFusion. Utukope tonse twa bomfiwe panuma ya kupoka insambu ku bene